File

To be Checked Against Delivery

# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

**HOTUBA YA**

**DK. SALIM AHMED SALIM**
**MWENYEKITI WA TAASISI YA MWALIMU NYERERE**

**MGENI RASMI KWENYE**

**SHUGHULI YA KUTUNZA TUZO YA ZEZE KWA WATENDAJI MAHIRI KATIKA SEKTA YA UTAMADUNI**

IJUMAA, 10 DESEMBA 2004
UKUMBI WA KARIMJEE
**DAR ES SALAAM**

**HOTUBA YA MGENI RASMI<br>MHESHIMIWA DR. SALIM AHMED SALIM,<br>MWENYEKITI WA MFUKO WA MWL. NYERERE<br>KWENYE SHUGHULI YA KUTUNZA TUZO YA ZEZE<br>KWA WATENDAJI MAHIRI KATIKA<br>SEKTA YA UTAMADUNI**

**Ndugu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Utamaduni Tanzania, Prof. Amandina Lihamba**

**Waheshimiwa Wafadhili wa Mfuko wa Utamaduni Tanzania**

**Waheshimiwa Mabalozi wa nchi mbalimbali**

**Ndugu Mkurugenzi wa Utamaduni**

**Waheshimiwa Wadhamini wa Mfuko**

**Waheshimiwa Wageni Waalikwa**

**Wasanii Washiriki katika Maonyesho**

**Waandishi wa Habari**

**Mabibi na Mabwana**

Awali ya yote natoa shukrani za dhati kwa Profesa Amandina Lihamba Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini wa Mfuko wa Utamaduni Tanzania na viongozi wenzake kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika kutoa Tuzo ya Zeze. Napenda kuwapongeza watunukiwa wa tuzo hii ya heshima kwa uaminifu na ujasiri wao katika kulinda na kuenzi utamaduni wetu.

***Waheshimiwa Wageni waalikwa,***

Hivi sasa dunia nzima inazungumzia mfumo wa utandawazi. Hili ni jambo ambalo halikwepeki. Mengi yanayozungumzwa kuhusu utandawazi yanasisitiza uzuri wake, manufaa yake na kadhalika. Ni kweli kuna mazuri mengi katika mfumo wa utandawazi lakini yale yaliyo na madhara yana ncha kali yenye uwezo wa kusababisha makovu ya kudumu. Watetezi wa utandawazi wanadai kwamba hakuna njia mbadala ya maendeleo nje ya mfumo wa utandawazi.

Kama kweli hakuna njia mbadala basi hatuna budi kuulinda utamaduni wetu kwa sababu huu una uwezo wa kuwa ngao imara ya kutukinga na kuhimili vishindo vya madhara yatokanayo na baadhi ya tamaduni za nje ambazo zinaingia kwa kasi kutokana na mfumo wa utandawazi.

Mfano ulioonyeshwa na wenzetu hawa waliotunukiwa leo unastahili kuigwa na kuendelea kuenziwa katika jamii yetu. Hii ni njia muhimu ya kuhimiza wananchi kuthamini kilicho chetu; yaani utamaduni wetu. Hapa ninazungumzia utamaduni katika maana pana inayojumuisha: kuendeleza lugha zetu za asili na hasa Kiswahili kinachotuunganisha, kuendeleza utaalam na ufundi asilia ambao unawezesha wataalam wetu kubuni na kutengeneza vifaa mbalimbali kama mikeka, vikapu, vyungu, marembo na mapambo, picha za kuchora, maumbo, zana za kilimo, uandishi wa vitabu vya kiada, hadithi, historia na mambo mengine mengi yenye manufaa kwa jamii.

Ningependa kuweka msisitizo kwenye uwekaji na utunzaji wa kumbukumbu kimaandishi. Vitabu vingi vinavyozungumzia historia ya nchi yetu tangu zama za

ukoloni vimeaandikwa na wageni. Matokeo ni kwamba wanaandika kutokana na mtazamo wao kwa hiyo mambo ya msingi; yaani yale yenye maana katika jamii yetu huachwa au kupuuzwa. Kwa hiyo watoto wetu wanaposoma historia wanapata mtazamo tofauti na hali halisi ilivyokuwa.

Kama wananchi wangejituma kuandika vitabu au hata kujitahidi kuweka katika kumbukumbu ya kudumu matukio muhimu katika nchi tungeweza kusahihisha yale yasiyo sahihi. Licha ya historia, kuna taalumu nyingi za asili zinazopotea kwa sababu haziko katika kumbukumbu ya kudumu. Tunategemea kurithishwa kwa kuangalia au kufundishwa na babu au bibi. Sasa vijana wengi wanakimbilia mijini au muda wao mwingi wapo shule hivyo hawana nafasi hata ya kusikiliza hadithi za bibi na babu ambazo zilikuwa na mafundisho mazuri sana. Nafasi ya bibi na babu imechukuliwa na Televisheni na Radio.

Ili kuweza kwenda na wakati tunatoa changamoto kwa waandishi na wabunifu, kuandika na kuandaa vitabu na programu za Televisheni na radio ambavyo vitaendeleza yale yaliyo mazuri katika utamaduni wetu, pamoja na kuhifadhi mambo muhimu katika kumbukumbu za kudumu.

***Waheshimiwa Wageni Waalikwa***

Kimsingi ninafarijika sana na jitihada zinazofanywa na Mashirika au Taasisi mbalimbali kuendeleza urithi na utambulisho wetu kama Taifa. Ni hivi majuzi tu nilialikwa kwenye uzinduzi wa kamusi ya Kiswahili. Tukio lile lilikuwa na burudani lakini kilichonifurahisha zaidi ni maelezo yaliyotolewa na wataalamu kuhusu matumizi ya maneno ya Kiswahili

na chimbuko la neno Kamusi. Maelezo ya neno kamusi yalitolewa na Mzee Andanenga, kwa jina la kishairi Sauti ya Kiza. Nimeelezwa kwamba huyu alitunukiwa Tuzo ya Zeze mwaka jana 2003.

Ninaamini jitihada za wadau na wapenzi wa utamaduni ndizo zilizowezesha lugha yetu ya Kiswahili kutambulika kama lugha yenye nafasi katika ngazi za kimataifa. Hili ni jambo la kujivunia. Lakini tuna kazi kubwa mbele yetu. Tunahitaji vitabu vingi vilivyoandikwa kwa lugha ya kiswahili ili tuweze kutosheleza mahitaji ya soko ambalo sasa linapanuka kwa kasi. Tusiache kazi hii ifanywe na watu wengine peke yao kwa sababu hatari ya kuua uasili au utamaduni unaoambatana na lugha. Tunahitaji wataalam wa kutafsiri katika mikutano ya kitaifa na kimataifa. Vile vile wataalamu wa kutafsiri vitabu vilivyoandikwa kwa lugha nyingine ili wananchi wetu waweze kujisomea na kujifunza maarifa yaliyo katika jamii nyingine duniani.

Utamaduni ni uwanja mpana unaogusa kila sekta na kila mtu katika nchi yetu. Si jambo la kudharauliwa. Ni sekta ya kuheshimiwa, kulelewa, kuenziwa, na kuendelezwa. Utamaduni ndio utambulisho wetu; utu wetu; kielelezo kinachoimarisha utashi wa Taifa letu.

Wenzetu waliopata tuzo leo wamekuwa mstari wa mbele katika kutetea utamaduni wetu kwa vitendo. Kwa mara nyingine tena napenda kuwapongeza.

***Waheshimiwa Wageni Waalikwa,***
Katika maisha yangu ya utumishi wa Taifa letu, nimepata fursa kubwa ya kuishi katika nchi mbalimbali za nje kwa muda wa miaka mingi.

Nimeishi Misri, India, China na Marekani. Pia nimetembelea takriban nchi zote za Kiafrika na idadi kubwa ya nchi za dunia. Jambo mojawapo ambalo nimejifunza kutokana na kuishi au kutembelea huko, ni jinsi gani nchi mbalimbali na jamii zake zinavyothamini, kuendeleza na kuheshimu utamaduni wake. Kwani utamaduni ni sehemu muhimu ya uhai na maendeleo ya kila taifa. Sisi Watanzania tumebahatika kuwa na utamaduni mkubwa na wa kale unaoambatana na mila mbalimbali za watu wetu. Utajiri huu sio tu wa kuthaminiwa na kutukuzwa lakini ni muhimu kulindwa, kudhibitiwa na kuendelezwa. Nataka kuchukua nafasi hii kutoa pongezi za moyoni kwa Mfuko wa Utamaduni Tanzania kwa juhudi zake zenye lengo la kufanikisha haya.

Mwisho, lakini hili ni la muhimu sana, Serikali yetu imetuundia sera ya utamaduni; inayoeleza majukumu ya Serikali Kuu, Serikali za Mikoa na Wilaya, majukumu ya wananchi na majukumu ya asasi na taasisi zisizo za Kiserikali katika kuendeleza utamaduni. Natoa wito kwa wananchi na viongozi wenzangu tusome kitabu cha Sera ya Utamaduni na kila mmoja wetu ashiriki kikamilifu katika kulinda na kuendeleza utamaduni Tanzania.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.